



**SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR
WIZARA YA AFYA,**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSIANA NA HUDUMA YA CHANJO KWA
MAHUJAJI WANAOTARAJIWA KWENDA KUHIJI 2023.
TAREHE 19/05/2023**

Ndugu Wananchi, Wizara ya Afya inatambua uwepo wa msimu wa hijja ya mwaka 2023, mahujaji wanatakiwa kuchanja chanjo nne kwa jumla ya dozi 6.

Chanjo hizo ni pamoja na chanjo ya Uviko-19 dozi moja (Covid-19 vaccine), chanjo ya homa ya manjano dozi moja (yellow fever vaccine), chanjo ya homa ya uti wa mgongo dozi moja (meningitis vaccine) na chanjo za homa ya ini dozi tatu (hepatitis vaccine).

Utoaji wa chanjo hizi zinatolewa kwa utaratibu maalum kwa kuzingatia aina ya chanjo na muda kwa mujibu wa makundi ya taasisi hizo yanavoondoka ili kuhakikisha kwamba mahujaji wote wanapata huduma hii kwa wakati.

Wizara ya Afya imeanza na inaendelea kutoa huduma za chanjo hizo kwa mahujaji wa taasisi zote za hijja Zanzibar ambao kwa mwaka huu wanakadiriwa kuwa takriban 2,300, na hadi sasa huduma hiyo imeshawafikia zaidi ya asilimia 51% sawa na mahujaji 1,173 kutoka Zanzibar.

Ndugu wananchi napenda kuwahakikishia kwamba Serikali imejipanga kuwahudumia mahujaji kwenye suala la chanjo na mahujaji watapata chanjo zote wanazostahiki kwa wakati.

Katika kuhakikisha hilo, wahudumu wetu wanatoa huduma katika kituo chetu cha chanjo kwa wasafiri Wizara ya afya na nje ya kituo chetu katika maeneo ya taasisi za hijja wakati wa semina zao ili kupunguza msongamano na kutoa huduma hiyo kwa ufanisi.

Aidha, kumekua na malalamiko kutoka kwa baadhi ya Wananchi kutokupatiwa chanjo kwa muda wanaotaka lakini hii inasababishwa na kutokua na uelewa wa kutosha juu ya chanjo husika na kutokufuata maelekezo yanayotolewa kutoka kwenye taasisi zao pamoja na kituo chetu cha chanjo.

USHAURI

Serikali inawataka mahujaji kua na utulivu wa kwamba kila hujaji atapatiwa chanjo zake zote kwa wakati.

Maswala ya chanjo ni maswala ya kitaalamu, hivyo tunawaomba Mahujaji waache kusikiliza kauli za mitaani na badala yake wasikilize ushauri na maelekezo wanayopewa kutoka kwa wataalamu wetu wa afya.

Ndugu wananchi mwisho kabisa kwa niaba ya Wizara ya Afya Zanzibar inawatakia mahujaji wote hijja njema.

**NASSOR AHMED MAZRUI,
WAZIRI WA AFYA,
ZANZIBAR.**